JARIDA LA ESHI LA POLISI TANZANIA

TOLEO LA TATU

MACHI 27-APRILI 3, 2020

Jarida hili limeandaliwa na Ofisi ya Uhusiano, Makao Makuu ya Polisi Dodoma

Umoja wetu ndio nguvu yetu.

TAHARIRI/ MAONI

Ni mategemeo yetu kuwa msomaji wa jarida hili la mtandaoni utaendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kutatua matatizo na kero mbalimbali za kiuhalifu nchini baada ya kusoma habari na makala mbalimbali zilizoandikwa kwenye jarida hili na wataalam mbalimbali kutoka ndani na nje ya Jeshi la Polisi.

Ifahamike kwamba mawazo, maoni na makala zilizoandikwa humu hazibebi msimamo wa Jeshi la Polisi isipokuwa ni uwasilishaji wa hoja, mitazamo na mawazo ya watu mbalimbali wakiwemo viongozi wakuu wa Jeshi la Polisi yenye lengo la kuielimisha, kuionya kuihabarisha na kuiburudisha jamii.

Jarida limetoa nafasi ya kupokea mawazo na taarifa kutoka kwa wadau mbalimbali na wasomaji wengine. Mhariri Mkuu anatoa nafasi ya kutoa ushauri, maoni na mapendekezo ambayo yatalete mchango chanya wa kuendeleza mjadala wa kutimiza lengo la kuhabarisha, kuelimisha, kuonya, kuadhibu na kuburudisha ili kuwa na taifa lenye ustawi wa uchumi bila uhalifu.

Kwa kutumia jarida hili tunaweza kuihamasisha jamii kuungana na Jeshi la Polisi katika kuzuia, kupambana na kutanzua uhalifu.
Tunawaalika wadau mbalimbali kutoa mchango wenu, hoja na mawazo yatakayowezesha kuimarisha usalama, amani na utulivu nchini.
Nimatarajio yetu kuwa ubia kati ya Jeshi la Polisi utaimarika zaidi baada ya kusoma jarida hili.

Asante sana, nikutakie usomaji mwema.
Umoja wetu ndio nguvu yetu

David A. Misime- SACP
Mhariri Mkuu

Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini IGP Simon Sirro, akiwapungia mikono baadhi ya wananchi wa Kakola Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wakati alipofanya ziara wilayani humo na kuzungumza na wananchi akiwataka kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi na kutoa taarifa sahihi kuhusiana na uhalifu na wahalifu, ambapo baada ya ziara hiyo ilifanyika Operesheni kubwa katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na kufanikiwa kukamata watuhumiwa wengi waliokuwa wakijihusisha na mauaji kwa kukata mapanga, wagange ambao ni wapiga ramli chonganishi na kukamata silaha mbalimbali.

TUSIWAACHE PEKEE YAO, NI WENZETU TUWASAIDIE

Na. PC Tamimu Adam

Kutoa ni moyo, ni msemo unaotumika kuhamasisha watu, vikundi mbalimbli ndani ya jamii kusaidia watu wenye uhitaji au waliopatwa na matatizo kwa ajili ya kuwafariji ili waone kuwa kuna watu ndani ya jamii wameguswa na shida zao licha ya juhudi za Serikali zinazofanyika.

Kwa kutambua umuhimu wa msemo huo, Mtandao wa Polisi wanawake Tanzania (TPF-net)chini ya Mwenyekiti wake Naibu Kamishna wa Polisi (DCP)Maria Nzuki, wameitaka jamii kuguswa na kuwasaidia watu wenye uhitaji kwa kuwasaidiavitu mbalimbali ikiwemo vyakula ili viweze kuwasaidia kuendesha maisha yao.

Hivi karibuni vyombo vya habari vimeripoti maafa ya mafuriko yaliyotokea Rufiji ambapo zaidi ya kata sita za Wilaya ya Kibiti zimekosa makazi baada ya nyumba zao kusombwa na maji kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali hapa nchi.Mafuriko hayo yameharibu barabara mbalimbali za Wilaya hiyo ikiwemo inayotoka Kibiti kwenda katika eneo la Mradi wa umeme katika maporomoko ya Mto Rufiji ambako magari yenye vifaa yalikwama kwenye maji.

Akizungumzia sauala la mafuriko hayo Mbunge wa Rufiji (CCM), Mohamed Mchengerwa alisema msaada unaohitajika haraka kwa wakazi hao ni chakula na mbegu ili kuwawezesha wakulima kupanda mazao ya muda mfupi ili kuepukana na njaa inayoweza kuwakumba. Mchengerwa alisema baada ya mafuriko hayo, kaya hizo zilihamishiwa katika shule ya Msingi Mhoro na Majengo ya Serikali ya Chumvi, lakini eneo hilo pia likajaa maji huku kukiwa na tatizo la chakula. Kutokana na kuguswa na maafa ya mafuriko yaliyowakuta wakazi wa Rufiji, Mtandao wa Polisi Wanawake Tanzaniaulitoa msaada wa vyakula, mafuta na sabuni.

Akikabidhi msaada huo, Mwenyekiti wa Mtandao wa Polisi Wanawake Tanzania (TPF-Net), Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) Maria Nzuki alisema Mtandao huo umetoa msaada wa unga kilo 1000, maharage kilo 500, mafuta ya kula lita 120, sukari kilo 100 pamoja na boksi 18 za sabuni kwa ajili ya wahanga waliopatwa na mafuriko.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Juma Njwayo ameushukuru Mtandao huo kwa msaada waliotoa na kusema kuwa msaada huo utawasaidia sana kwa kuwa zaidi ya Hekari 4000 za mazao zimesombwa na maji hivyo kuongeza mahitaji ya chakula kwa wakazi waliokumbwa na mafuriko na kuwaomba wasichoke kusaidia watu wenye uhitaji mbalimbali kwa sababu ndani ya jamii watu wanatofautiana hali ya kiuchumi.

Mkurugenzi wa Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma, Ibrahim Maumi (aliyesimama mwenye koti jeusi) akitoa elimu kuhusiana na ubore shajimfumo wa kumbukumbu za utumishi wa umma kwa Maka mishnamaofisa Machi 24, 2020 Makao ya Jeshi la Polisi Dodoma.

JINSI YA KUJIKINGA NA VIRUSI VYA KORONA KWA KUNAWA MIKONO



POLISI KATAVI YAKAMATA MTAMBO WA KUTENGENEZA SILAHA

Na PC Daniel Kimaro

JESHI la Polisi Mkoa wa Katavi kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama Mkoa wa Katavi limemkamatamtu mmoja anayefahamika kwa jina la Emmanuel Mahanga maarufu kama Rambo[56] mzaliwa wanchi ya Burundi mkazi wa kijiji cha Busongola Wilaya ya TanganyikaMkoa wa Katavi akiwa anamiliki mtambommoja wa kutengeneza silaha haramu aina ya gobore na risasi zake.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi,Kamishna Msaidiziwa Polisi[ACP] Benjamin Kuzaga alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa tarehe machi 04,2020 majira ya jioni Kijijinikwake Busongola baada ya msako mkali uliofanywa na vyombo vya ulinzi na usalama, baada ya kupatataarifa toka kwa raia wema juu ya taarifa za mtuhumiwa huyo.

Baada ya taarifa hizo kupatikana kikosi kazi maalumu kilichoundwa na kamati ya ulinzi na usalama Mkoawa Katavi kinachofanya kazi ya kupambana na uhalifu, kilianza kufanya msako na kufanikiwa kumkamatamtuhumiwa huyo.Kamanda Kuzaga aliongeza kuwa mtambo huo aliokamatwa nao mtuhumiwa anautumiakwa ajili ya kuyeyushia vyuma na kisha kutengeneza silaha haramu aina ya gobore na risasi zake.

Pia katika upekuzi uliofanywa nyumbani kwa mtuhumiwa alikutwa na kipande kimoja cha ngozi ya mnyamapori aina ya nyati alichokuwaamekihifadhi ndani kwake na alipohojiwa alieleza kuwa ngozi hiyo huwa anaitumiakutengeneza dawa kwa ajili ya kufanya shughuli zake za uwindaji haramu.Silaha hizo haramu zimekuwazikitumika kufanya shughuli haramu za ujangili kwa kuua wanyama pori kwenye hifadhi ya Taifa yaKatavi na maeneo ya mapori ya akiba. kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama Mkoa wa Katavi limemkamata mtu mmoja anayefahamikakwa jina la Emmanuel Mahanga maarufu kama Rambo[56]mzaliwa wa nchi ya Burundi mkazi wakijiji cha Busongola Wilaya ya Tanganyika Mkoa wa Katavi akiwa anamiliki mtambo mmoja wa kutengenezasilaha haramu aina ya gobore na risasi zake.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi,Kamishna Msaidiziwa Polisi[ACP] Benjamin Kuzaga alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa tarehe 04.3.2020 majira ya jioni Kijijinikwake Busongola baada ya msako mkali uliofanywa na vyombo vya ulinzi na usalama, baada ya kupatataarifa toka kwa raia wema juu ya taarifa za mtuhumiwa huyo.

Baada ya taarifa hizo kupatikana kikosi kazi maalumu kilichoundwa na kamati ya ulinzi na usalama Mkoa.

Kamishna wa Ushirikishwaji wa Jamii [CP] Dkt. Mussa A. Mussa (kulia) akipata maelezo ya hali ya usalama katika daraja la Kiyegea kutoka kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) Wilbroad Mutafungwa machi 26,mwak huu

Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi [SACP] David Misime, akipimwa joto la mwili kabla ya kuingia Ofisini kwake Makao Makuu ya Jeshi hilo jijini Dodoma Machi 26, mwaka huu.

ASKARI POLISI ALIYETUNUKIWA UDAKTARI WA HESHIMA APANDISHWA CHEO

Na A/INSP Abdallah Nyambi

Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) Simon Nyakoro Sirro amempandisha cheo askari WP. 7490 PC CHRISTINA NABOTH ONYANGO kuwa Mkaguzi Msadidizi wa Polisi (A/Inspector) kutoka cheo cha Konstebo wa Polisi (PC).WP 7490 Pc Christina Naboth Onyango tarehe 22, Februari 2020 alitunukiwa shahada ya Udaktari(DOCTOR OF HUMANITY) na Chuo Kikuu cha LEAD IMPACT kilichopo nchini Marekani kutokanana utendaji wake mzuri uliotukuka.

Askari huyu alitoa wazo la kuanzishwa kituo cha huduma kwa pamoja yaani “ONE STOP CENTRE” kati ya Jeshi la Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam na taasisi zingine za Serikali zinazojishughulisha na masuala ya kupinga ukatili wa Kijinsia ambacho kipo katika Hospitali ya Amana Manispaa ya Ilala Jijini DSM.

Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini IGP Simon Nyakoro Sirro mnamo tarehe 11, Machi ,2020 alimponge zakwa barua na kumpandisha cheo kuwa Mkaguzi Msaidizi wa Polisi na kumuelekeza Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam SACP lazaro Mambosasa kumvalisha cheo hicho.

Mnamo tarehe 26, Machi,2020 Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam SACP Lazaro Mambsasa amemvisha cheo askari WP 7490 PC Christina Naboth Onyango kuwa Mkaguzi msaidizi wa Polisi na kumpongeza kwa kuliwakilisha Jeshi la Polisi vizuri katika Jamii

Kamanda wa Polisi mkoa wa Morogoro Kamishna Msaidizi Mwand amizi(SACP)Wilbroad Mutafungwa kushoto akiwa na Mhandisi Boni-faceMkumbo ambaye ni msimamizi Mkuu wa ujenzi wa daraja la kiyegea mkoani Morogoro baada kutembelea kwenye daraja hilo Machi 26 mwaka huu.

Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Salehe Manjoti aliyesimama katikati aki toamaelekezo kwa Askari wa kitengo cha ulinzi wa jengo lililokuwa Makao Makuu ya Polisi Dar es Salaam mara baada ya kumaliza maoezi ya utayari Machi 26, 2020 yaliyofanyika kwa muda wa mwezi mmoja.

FAHAMU MAKOSA YA MTANDAO

Na.SP Joshua Mwangasa

Maana ya Makosa ya Mtandao
Ni kutenda kitendo kinyume na mwenendo wa Makosa ya Jinai, ambapo kifaa cha ki-elektronia au mfumo wa kompyuta unaweza/kinaweza kutumika kama kifaa cha kutendea kosa au kitendewa kosa(use as a tool or Target). Makosa ya mtandao ni Makosa kama makosa mengine isipokuwa yamekuja na sura mpya yautendaji wa makosa(Modus Operand).

> Kwa nini watu hufanya uhalifu kutumia mitandao ya kijamii.

- Kukosa hofu ya Mungu
- Ukosefu wa maadili
- Kujipatia kipato
- Kukosekana na kanuni na taratibu za kueleweka.mf,makundi ya Whatsap
- Ni rahisi kupata kwa taarifa na kuzifikish
- Ni suala mtambuka
- Ni rahisi kuingia
- Haina gharama
- Wanafikiri watakuwa salama kutoka kwenye mikono ya dola
- Kutafuta umaarufu
- Kwa ajili ya kijifurahisha

> Baadhi ya Makosa yanayofanyika kwenye Mitandao ya KijamiiTanzania

- Kuingilia mawasiliano kinyume cha sheria.
- Kuingilia data kinyume cha sheria.
- Ujasusi data.
- Matumizi ya mfumo wa kompyuta kinyume cha sheria.
- kutumia Kifaa cha mawasiliano kisicho halali.
- Udanganyifu unaohusiana na kompyuta.
- Kugushi kunakohusiana na masuala ya Kompyuta.
- Ponografia ya watoto
- Ponografia
- Makosa yanayohusiana na utambuzi.
- Kutoa taarifa za uongo.Kutoa taarifa za uongo.